

## Maswali

1. Ni kwa nini Yakobo alikimbia nyumbani aende Harani?
2. Yakobo alikutana na nani kando ya kisima?
3. Labani alikuwa nani kwa Yakobo?
4. Kwanza Yakobo alimfanyia Labani kazi kwa muda gani ili amwoe Raheli?
5. Yakobo alipofikiri anamwoa Raheli, ni nani hasa alikuwa akimwoa?
6. Labani alisema ni kwa nini alimfanyia Yakobo ujanja huo?
7. Jumla ya miaka ngapi yenyeye Yakobo alifanya kazi kwa Labani ili ampate Raheli?
8. Yakobo alikuwa na wana wangapi?
9. Yakobo na wanawe walienda wapi walipotoka Harani?
10. Hawa watu walikuwa ni mababa wa akina nani?

## Majibu

1. Yakobo alikimbia aende Harani kwa sababu Esau alipanga kumwua
2. Yakobo alikutana na Raheli kando ya kisima
3. Labani alikuwa mjomba wa Yakobo
4. Kwanza Yakobo alimfanyia Labani kazi kwa muda wa miaka saba.
5. Yakobo alimwoa Lea akifikiria ni Raheli.
6. Labani alisema, kwa desturi yao binti mdogo, hawawezi kuolewa mbele ya mkubwa.
7. Kwa jumla, Yakobo alifanya kazi kwa muda wa miaka kumi na minne ili ampate Raheli.
8. Yakobo alikuwa na wana kumi na wawili.
9. Yakobo na wanawe walienda nchi ya Kanaani (iliyoahidiwa Ibrahimu na uzao wake).
10. Hawa watu walikuwa mababa wa kabilo kumi na mbili za taifa la Israeli

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM



**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

## 10 Yakobo akafanya kazi kwa Labani

### Marejeo

Mwanzo 28 + 29



### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba kuoa kwa imani moja ni vyema. Na kuona vile Yakobo alidanganya naye akadanganya.

### Maneno maalum

1. Esau alichukia Yakobo + Yakobo akaenda Harani + Kukutana na Raheli.
2. Labani + Kuishi kwa Yakobo + Anataka Raheli + Miaka saba.
3. Labani anadanganya Yakobo + Lea apeanwa.
4. Miaka mingine saba + anaoa Raheli
5. Anarudi Kanaani + Amani.

**10.1** Esau alikasirika mno kwa vile hakupokea baraka kwa Isaka. Esau akapanga kumuua Yakobo. Isaka na Rebeka wakampeleka kwenda kukaa na jamaa ya Rebeka ilio ishi Harani. Kulikuwa na hatari nyingi njiani lakini Mungu alikuwa pamoja na Yakobo, akamleta salama hadi Harani.

Yakobo akafika kunako kisima kile kilicho nje ya mji wa Harani, ambacho Rebeka aliwatekeea maji ngamia wa Eliezeri. Yakobo akafika kisimani, aliwaona wachungaji watatu na makundi yao ya kondoo. Wachungaji walisubiri kuwapa maji kondoo wao katika kisima. Yakobo aliuliza iwapo walimjua mjomba wake Labani (kaka wa Rebeka). Mara mwanamwali alikuwa akija kisimani pamoja na kundi la kondoo. "Huyu ni Raheli, bintiye Labani," wachungaji walimwambia Yakobo.

**10.2** Yakobo alifurahi sana kumuona mpwa wake Raheli. Yakobo alichoka sana kutokana na safari yake ndefu, lakini aliwapa kondoo wote wa Raheli maji. Basi Raheli alikimbia kumuarifu Labani ya kwamba mwana wa Rebeka amekuja Harani. Labani alimkaribisha kukaa nao. Yakobo alikaa na Labani kwa majuma manne akimsaidia kuchunga mifugo wake. Ndipo Labani akamuuliza mshahara gani angependa kwa kazi yake. Labani alikuwa na binti wawili, Lea na Raheli. Binti mdogo Raheli alikuwa mzuri sana na Yakobo kampenda. Yakobo akamwambia Labani kwamba alitaka kumwoa Raheli. Yakobo alikubali kumfanyia kazi kwa miaka saba kulipa mahari ya Raheli. Labani alifurahi sana kwa mwafaka (mapatano) huu.

Yakobo alifurahi kwamba atamwoa Raheli baada ya miaka saba. Alifanya kazi sana kwa miaka saba. Alikuwa mchungaji mwema. Miaka ilipita haraka sana kwa sababu alimpenda Raheli mno.

**10.3** Miaka saba ilipoisha, Yakobo alimwambia Labani ya kwamba alitaka amwoe Raheli. Labani alianda siku kuu kubwa ya arusi itakayo dumu juma moja. Yakobo alifurahi kwamba Raheli atakuwa mke wake punde. Katika nchi ile kulikuwa desturi kwa binti mkubwa kuwa wa kwanza kuolewa. Labani alitaka Lea aolewe kabla ya Raheli. Labani hakumwambia Yakobo. Badala yake alimfanyia hila. Labani akamvika Lea kama bi arusi. Ilikuwa desturi kwa mwanamke kucaa shela kufunika uso wake. Yakobo hakuweza kuuona uso wa Lea. Aliwaza ya kwamba alikuwa anamwoa Raheli. Yakobo hakuweza kujua kwamba bi arusi alikua Lea hadi walipoona.

**10.4** Yakobo alikasirika sana kwamba Labani alimdaganya. Yakobo alifanya kazi sana miaka saba ili kumwoa Raheli. Badala yake alimwoa Lea. Labani alikubali kwamba atamwoa Raheli baada ya juma la sherehe ya kumwoa Lea. (Katika siku hizo, wanaume waliruhuswa kuwa na wake wengi). Yakobo alikubali kufanya kazi kwa miaka saba mingine kulipia mahari ya Raheli. Yakobo alimpenda sana Raheli hata alipenda kufanya kazi miaka kumi na mine kwa ajili yake.

**10.5** Yakobo akawa na watoto kumi na wawili wakati akiishi Harani. Wote wakawa walizaliwa na Lea na Raheli na wajakazi wao. Mungu alimwambia Ibrahim ya kwamba uzao wake utakua taifa kubwa. Wana kumi na wawili wa Yakobo wakawa ni kabilia kumi na mbili. Kabilia hizi kumi na mbili zikawa taifa la Israeli. Mungu alikuwa akitenda kazi katika maisha ya Yakobo kwa kutimiza ahadi na Baraka alizotoa.

**10.6** Baada ya miaka ishirini, Yajobo alirudi kuishi nchi ya Kanaani. Alifanya amani na ndugu-kaka yake-Esau. Aliishi nchi ya Kanaani. Hii ndiyo nchi ambayo Mungu alimwahidi Ibrahim na uzao wake milele.